JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA KILIMO

TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA TANZANIA

MWONGOZO WA UHAMASISHAJI NA UANZISHAJI WA VYAMA VYA USHIRIKA

IMEANDALIWA NA;

TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA

S.L.P 201

DODOMA

TOLEO LA PILI JULAI 2026

DIBAJI

Vyama vya ushirika vimeendelea kuwa chombo muhimu cha kuwaunganisha wananchi ili kukabiliana na changamoto za kijamii na kiuchumi kupitia misingi ya kujitegemea, umiliki wa pamoja, ushiriki wa kidemokrasia na mgawanyo wa manufaa kwa wanachama.

Katika kipindi chote cha maendeleo ya Taifa, sekta ya ushirika imeendelea kutoa mchango mkubwa katika kukuza uchumi, kuongeza ajira, kuimarisha usalama wa chakula, kuwezesha upatikanaji wa huduma za kifedha, kuimarisha masoko ya bidhaa na huduma pamoja na kuboresha maisha ya wananchi. Kutokana na umuhimu huo, Serikali imeendelea kuboresha mazingira ya kisera, kisheria na kiutawala ili kuwezesha sekta ya ushirika kuchangia kikamilifu katika utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, Mpango wa Taifa wa Maendeleo na mikakati mingine ya maendeleo ya Taifa.


Katika kuimarisha usimamizi na maendeleo ya sekta ya ushirika, Serikali imefanya maboresho katika Sheria ya Vyama vya Ushirika (Sura ya 211) iliyoanzisha Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania. Kwa mujibu wa Sheria hiyo, Tume imepewa jukumu la kusimamia na kuhamasisha shughuli za ushirika nchini kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na wadau wengine wa maendeleo.

Aidha, Sheria hiyo imeweka masharti ya uanzishaji, usajili, uendeshaji, usimamizi na maendeleo ya Vyama vya Ushirika nchini. Baada ya kuanzishwa kwa Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS), vinapaswa kutoa huduma ikiwa vimepatiwa leseni kwa mujibu wa Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha (Sura ya 407) na kanuni zake za mwaka 2019

Pamoja na jitihada hizo, bado kuna changamoto zinazohusiana na uelewa mdogo wa dhana, misingi, maadili na faida za ushirika katika baadhi ya maeneo nchini. Changamoto hizo zimechangia kupunguza kasi ya uanzishwaji wa vyama vipya vya ushirika, ushiriki mdogo wa baadhi ya makundi ya wananchi hususan vijana, wanawake na watu wenye ulemavu pamoja na uwepo wa baadhi ya vyama vinavyoshindwa kujiendesha kwa ufanisi.

Kwa kuzingatia umuhimu huo, Tume ya Maendeleo ya Ushirika imeandaa Mwongozo huu wa Uhamasishaji na Uanzishaji wa Vyama vya Ushirika ili kutoa mwongozo kwa wahamasishaji, Maafisa Ushirika, Wizara za Kisekta, Mamlaka za Serikali za Mitaa, taasisi mbalimbali na wadau wengine kuhusu taratibu na mbinu bora za kuhamasisha wananchi kuanzisha na kujiunga na Vyama vya Ushirika.

Ni matumaini yangu kuwa mwongozo huu utakuwa nyenzo muhimu katika kuimarisha uratibu wa shughuli za uhamasishaji na uanzishaji wa Vyama vya Ushirika nchini, kuongeza ushiriki wa wananchi katika shughuli za kiuchumi kupitia ushirika na kuchangia maendeleo endelevu ya sekta ya ushirika kwa manufaa ya wanachama na Taifa kwa ujumla.



Dkt. Benson O. Ndiege

MRAJIS WA VYAMA VYA USHIRIKA

YALIYOMO

DIBAJI 2
SEHEMU YA KWANZA 7
1.0 UTANGULIZI 7
1.1 MAMLAKA YA KUANDAA MWONGOZO 7
SEHEMU YA PILI 8
2.0 MALENGO NA WALENGWA WA MWONGOZO 8
2.1 MALENGO YA MWONGOZO 8
2.1.1 LENGO KUU 8
2.1.2 MALENGO MAHUSUSI 8
2.2 WALENGWA WA MWONGOZO 8
SEHEMU YA TATU 9
3.0 UHAMASISHAJI WA VYAMA VYA USHIRIKA 9
3.1 Sifa za mhamasishaji 9
3.2 Kutambua mahitaji kwa kuzingatia Mazingira husika 9
3.3 Maandalizi ya Mada 9
3.4 Njia za kufanya uhamasishaji 9
3.5 Maeneo katika uhamasishaji 10
3.6 Hatua muhimu za kuzingatia wakati wa uanzishaji wa Chama cha Ushirika 10
3.6.1 Kufanya uamuzi wa hiari 10
3.6.2 Kuitisha na kufanya Mkutano wa Awali 10
Majukumu ya Kamati anzilishi ni pamoja na; 11
3.6.3 Mkutano wa kujadili mapendekezo ya Kamati Anzilishi 11
3.6.4 Kuwasilisha maombi ya kuandikisha Chama 11
3.6.5 Taratibu za Utoaji wa Leseni kwa Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS) 12
3.6.6 Mkutano Mkuu wa kwanza baada ya Chama kuandikishwa 12
3.6.7 Taratibu za uchaguzi wa bodi baada ya Chama kuandikishwa 13
3.7 Uhamasishaji wa Vyama vya Ushirika Sinzia 13
3.8 Uendelezaji wa Vyama vya Ushirika. 13
3.8.1 Umiliki wa Wanachama 14
3.8.2 Udhibiti wa Wanachama 14

3.8.3 Ushiriki wa Wanachama 14
SEHEMU YA TANO 15
5.0 HITIMISHO 15
VIAMBATISHO 16
Kiambatisho Na. 1 16
1. DHANA YA USHIRIKA 16
1.1 Ushirika kama Dhana 16
1.2 Maana ya Ushirika 16
1.3 Maadili ya Ushirika 16
1.4 Misingi ya Ushirika 16
1.5 Ushirika kama Taasisi 17
Kiambatisho Na. 2 18
2.0 AINA YA VYAMA VYA USHIRIKA VINAVYOWEZA KUANZISHWA 18
2.1 Ushirika wa Kilimo na Masoko (Agricultural Marketing Cooperative Society): 18
2.2 Ushirika wa Akiba na Mikopo (Savings and Credit Cooperative Society-SACCOS): 18
2.3 Ushirika wa Waalaji (Consumer Cooperative Society): 18
2.4 Ushirika wa Viwanda (Industrial Cooperative Society): 18
2.5 Ushirika wa Nyumba (Housing Cooperative Society): 19
2.6 Ushirika wa Mifugo (livestock Cooperative Society): 19
2.7 Ushirika wa Uvuvi (Fisheries Cooperative Society): 19
2.8 Ushirika wa Madini (Mining Cooperative Society): 19
2.9 Ushirika wa Benki (Cooperative Bank): 19
Kiambatisho Na. 3 21
3. Wajibu na Haki ya Mwanachama 21
3.1 Wajibu 21
3.2 Haki 21
Kiambatisho Na. 4 22
FOMU YA TATHMINI YA UWEZO WA KIUCHUMI ("VIABILITY ASSESSMENT FOR COOPERATIVE SOCIETY") WA CHAMA CHA USHIRIKA. 22
SEHEMU YA KWANZA 22
SEHEMU YA PILI 23

2.0 UANACHAMA: 23
Taarifa za Wanachama 23
3.0 MENEJIMENTI NA UWAJIBIKAJI 23
4.0 MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI 24
MAPATO 24
MATUMIZI 24
5.0 UWEPO WA MAHITAJI YA AWALI KUISAIDIA UFANISI 25
(a) Huduma mbalimbali 25
6.0 MATARAJIO YA KIJAMII NA KIUCHUMI 25
SEHEMU YA TATU 26
7.0 MAONI YA AFISA USHIRIKA WA WILAYA 26
8.0 MAONI YA MRAJIS MSAIDIZI WA VYAMA VYA USHIRIKA MKOA 26
SEHEMU YA NNE 27
UAMUZI WA MRAJIS WA VYAMA VYA USHIRIKA 27

SEHEMU YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

Tume ya Maendeleo ya Ushirika ina jukumu la kuhamasisha na kusimamia maendeleo ya Ushirika nchini kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wakiwemo Wizara za Kisekta, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na wadau wengine wa maendeleo ya Ushirika. Jukumu hili, linatekezwa kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika (Sura ya 211).

Kutokana na changamoto ya uhamasishaji na uanzishaji wa Vyama vya Ushirika bila kufuata taratibu kama zilizoainishwa kwenye Sheria ya Vyama vya Ushirika na Kanuni zake, kumekuwepo na vyama vya ushirika ambavyo havina uimara na uendelevu unaohitajika. Hivyo, ili kuhakikisha kuwa uhamasishaji na uanzishaji unafanyika kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Vyama vya Ushirika, Tume ya Maendeleo ya Ushirika imeandaa Mwongozo huu wenye lengo la kuwapatia wahamasishaji na wasimamizi uelewa wa pamoja kuhusu namna bora ya kutekeleza majukumu yao.

1.1 MAMLAKA YA KUANDAA MWONGOZO

Mrajis wa Vyama vya Ushirika Tanzania, kwa mujibu wa kifungu cha 8 cha Sheria ya Vyama vya Ushirika (Sura ya 211) na ikisomwa pamoja na Kanuni ya 81(1)(b) ya Kanuni za Vyama vya Ushirika za mwaka 2015 amepewa mamlaka ya kuandaa na kutoa miongozo na maelekezo yanayopaswa kuzingatiwa na Vyama vya Ushirika kwa ajili ya ustawi wa Sekta ya Ushirika.

SEHEMU YA PILI

2.0 MALENGO NA WALENGWA WA MWONGOZO

2.1 MALENGO YA MWONGOZO

2.1.1 LENGO KUU

Kuweka utaratibu maalum unaopaswa kuzingatiwa na wahamasishaji wote katika kutekeleza majúkumu yao ya uhamasishaji na uanzishwaji wa Vyama vya ushirika nchini.

2.1.2 MALENGO MAHUSUSI

i. Kuweka uelewa wa pamoja juu ya dhana ya Ushirika na uendeshaji wa Vyama vya Ushirika;
ii. Kuwezesha wahamasishaji kuzingatia taratibu za uanzishaji na usajili wa Vyama vya Ushirika kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika na Kanuni zake;
iii. Kuwezesha wahamasishaji kutumia mbinu mbalimbali za kuhamasisha jamii kuanzisha na kujiunga kwenye Vyama vya Ushirika vilivyopo; na
iv. Kurahisisha kazi ya uratibu wa majukumu ya uhamasishaji ili kutoa maelekezo na maamuzi yanayofanana kwa Vyama vyote vya Ushirika nchini.

2.2 WALENGWA WA MWONGOZO

Walengwa wa mwongozo huu ni pamoja na;

i. Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania;
ii. Wizara za kisekta;
iii. Tawala za mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;
iv. Vyama vya Ushirika;
v. Kamati za elimu za Ushirika;
vi. Taasisi mbalimbali za umma; na
vii. Sekta binafsi

SEHEMU YA TATU

3.0 UHAMASISHAJI WA VYAMA VYA USHIRIKA.

3.1 Sifa za mhamasishaji

Mhamasishaji anapaswa kuwa na sifa zifuatazo:-

i. Awe ni Afisa aliyeajiriwa na Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania, Wizara za kisekta, Sekretarieti za Mikoa au Mamlaka za Serikali za Mitaa;

ii. Awe na uelewa wa maswala ya ushirika kwa ujumla; **(Kiambatisho No 1)**

iii. Awe na uelewa wa mazingira ya kijamii, kiuchumi na kiutamaduni ya eneo husika;

iv. Awe na Uwezo wa kuwasiliana, kujadiliana na kushawishi jamii;

v. Awe na Uwezo wa kutumia TEHAMA katika uhamasishaji; na

vi. Awe na Uwezo wa kufuatilia na kutathmini matokeo ya uhamasishaji.

3.2 Kutambua mahitaji kwa kuzingatia Mazingira husika

Mhamasishaji kabla ya kwenda kwenye zoezi la uhamasishaji, anapaswa kuelewa mazingira ya sehemu husika na aina ya watu anaokwenda kuwahamasisha ili aweze kutoa elimu stahiki yenye matokeo chanya kwa lengo la kuwa na Ushirika imara na endelevu unaojibu mahitaji ya wananchi kwa kuzingatia shughuli za kiuchumi walizonazo.

3.3 Maandalizi ya Mada

Mhamasishaji anapaswa kuandaa mada mapema na kwa ufanisi ili kuhakikisha kunakuwepo na matokeo chanya. Mhamasishaji anapaswa kuwa na mwelekeo kwa kuzingatia aina ya Ushirika unaotarajiwa kuanzishwa **(Kiambatisho Na. 2)** kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Ushirika.

3.4 Njia za kufanya uhamasishaji

Ili kuwezesha uhamasishaji kutolewa ipasavyo, Mhamasishaji anatakiwa kutumia njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na: -

a) Vipeperushi;
b) Mihadhara na mikutano;
c) Majadiliano kwenye vikundi;

d) Kisa mkasa;
e) Ziara ya mafunzo;
f) Mitandao ya kijamii; na
g) Vyombo vya habari;

3.5 Maeneo katika uhamasishaji

Uhamasishaji hufanyika kwa mujibu wa Kifungu cha 8(2)(b) cha Sheria ya Vyama vya Ushirika (Sura ya 211), kwa lengo la kuwa na Vyama vya Ushirika imara na endelevu. Uhamasishaji unaweza kufanyika kwa kuzingatia mahitaji ya jamii husika ambapo:

i. Mhamasishaji anaweza kuangalia fursa zilizopo na kuwahamasisha wananchi juu ya uanzishwaji wa chama cha Ushirika; au
ii. Wananchi kwa hiari yao wenyewe waone umuhimu wa kuanzisha Chama cha Ushirika.

3.6 Hatua muhimu za kuzingatia wakati wa uanzishaji wa Chama cha Ushirika

Mchakato wa kuanzisha Chama Cha Ushirika unapaswa kuzingatia mambo yafuatayo;

3.6.1 Kufanya uamuzi wa hiari

Watu wanaokusudia kuanzisha chama cha ushirika watapaswa kufanya uamuzi wao kwa hiari. Wakishafanya uamuzi huo, watatoa taarifa kwa Afisa Ushirika wa eneo husika ili aweze kukutana nao na kuwapatia mwongozo/maelekezo ya mchakato wa namna ya uanzishaji wa chama cha ushirika wanachokusudia kuanzisha. Baada ya Mhamasishaji kutoa elimu ya Ushirika hana budi kuwapa muda wananchi ili watafakari kuhusu maamuzi ya aina ya ushirika watakaoweza/wanaotaka kuanzisha kutegemeana na mahitaji yao na mazingira yanayowazunguka.

3.6.2 Kuitisha na kufanya Mkutano wa Awali

Mkutano wa awali utafanywa chini ya usimamizi wa Afisa Ushirika ili kuchagua Kamati anzilishi ambapo miongoni mwao Mwenyekiti na Katibu watachaguliwa. Katika Mkutano huo, Afisa Ushirika atakuwa na majukumu yafuatayo:-

i. Kuwaelimisha wananchi wanaokusudia kuanzisha Chama cha Ushirika kuhusu dhana ya Ushirika, taratibu na kazi za kufanya ili kufanikisha uanzishaji wa Chama cha Ushirika;
ii. Atasimamia Mkutano anzilishi; na
iii. Mkutano huu utakasimu madaraka kwa Kamati Anzilishi kwa ajili ya kutekeleza majukumu yatakayowezesha kuandikishwa kwa chama.

Majukumu ya Kamati anzilishi ni pamoja na;

i. Kujadili kwa kina nia na madhumuni ya chama kinachotarajiwa kuanzishwa;
ii. Kuandaa orodha ya wanachama na mtaji kwa kuzingatia maazimio ya Mkutano wa Wanachama na kuandaa Masharti ya Chama;
iii. Kuitisha Mkutano Mkuu wa Uanzilishi;
iv. Kutayarisha taarifa ya uwezo wa kiuchumi wa Chama (kidadisi uchumi).
v. Kuandaa Mpango Biashara wa Chama;
vi. Kuandaa makisio ya Mapato na Matumizi (bajeti) ya Chama ya mwaka wa kwanza;
vii. Kuhamasisha wananchi wengine kujiunga na Chama hicho tarajiwa;
viii. kupokea viingilio, kupokea fedha za hisa na michango mingine kulingana na mahitaji ya Chama kama ilivyokubalika kwenye Mkutano wa uanzilishi;
ix. Kutafuta ofisi ya Chama pamoja na kununua vitendea kazi;
x. Kufanya mambo mengine yoyote yatakayowezesha kufanikisha mahitaji ya usajili wa Chama kama itakavyoshauriwa na Afisa Ushirika.

3.6.3 Mkutano wa kujadili mapendekezo ya Kamati Anzilishi

Baada ya Kamati anzilishi kukamilisha maandalizi yake, kamati hiyo itaitisha Mkutano wa uanzilishi kuhusu mapendekezo yaliyoandaliwa na Kamati. Mkutano huo, utasimamiwa na Afisa Ushirika na utafanya kazi kama zilivyoainishwa katika Kanuni ya 7(2) ya kanuni za Vyama vya ushirika ya mwaka 2015

3.6.4 Kuwasilisha maombi ya kuandikisha Chama

Maombi ya kuandikishwa kwa Chama cha Ushirika yatawasilishwa kwa Mrajis wa Vyama vya Ushirika kupitia Mfumo wa kieletroniki wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (MUVU).

Kamati Anzilishi kwa kushirikiana na Afisa Ushirika itawajibika kufanya maombi na kuingiza taarifa zote muhimu katika mfumo huo, ikiwemo taarifa za wanachama, masharti ya chama, mpango biashara, taarifa ya uwezo wa kiuchumi wa chama (kidadisi uchumi), makisio ya mapato na matumizi pamoja na nyaraka nyingine zinazohitajika kwa mujibu wa sheria. Mfumo wa MUVU utatumika kufuatilia hatua zote za maombi ya kuandikishwa.

Baada ya kupokea maombi na nyaraka zote zinazohitajika, Mrajis atazipitia ili kujiridhisha kuwa masharti yote ya kisheria yametimizwa kabla ya kufanya uamuzi wa kusajili au kutosajili chama husika.

3.6.5 Taratibu za Utoaji wa Leseni kwa Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS)

Baada ya usajili wa Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS) kukamilika kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika, chama hicho hakitaruhusiwa kuanza kutoa huduma za kifedha mpaka kipate leseni ya kufanya biashara ya huduma ndogo za fedha kwa mujibu wa Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha (Sura ya 407) na Kanuni zake. Hivyo, Viongozi wa SACCOS iliyosajiliwa itakuwa na wajibu wa kuomba leseni kwa Tume ya Maendeleo ya ushirika (Mamlaka kasimiwa) ili kupata leseni ya kufanya biashara ya fedha.

Katika hatua ya uhamasishaji na uanzishaji wa SACCOS, wahamasishaji na Maafisa Ushirika wanapaswa kuwaelimisha waanzilishi kuhusu masharti ya upatikanaji wa leseni, mahitaji ya mtaji wa chini, mifumo ya usimamizi wa fedha, utunzaji wa kumbukumbu, usimamizi wa vihatarishi, ulinzi wa amana za wanachama, pamoja na uzingatiaji wa matakwa yote ya Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha na Kanuni zake.

3.6.6 Mkutano Mkuu wa kwanza baada ya Chama kuandikishwa

Baada ya kuandikishwa kwa Chama cha ushirika, kamati anzilishi itakuwa na wajibu wa kuitisha Mkutano Mkuu wa kwanza utakaohudhuriwa na wanachama waanzilishi ambao watakuwa wamelipa Hisa na Kiingilio. Mkutano huo utafanyika ndani ya siku 60 tangu tarehe ya kuandikishwa kwa chama na utajadili masuala yaliyoainishwa katika Kanuni ya 41 ya Kanuni za Vyama vya Ushirika ya Mwaka 2015

3.6.7 Taratibu za uchaguzi wa bodi baada ya Chama kuandikishwa

Katika Mkutano mkuu wa kwanza baada ya Chama cha Ushirika kuandikishwa kwa mujibu wa Sheria, Chama kinapaswa kufanya uchaguzi wa viongozi wa Bodi na Kamati kwa mujibu wa Sheria, Kanuni, Miongozo na Masharti na Chama. Uchaguzi wa viongozi hao, utafanyika kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Waraka wa Mrajis unaohusu masuala ya uchaguzi.

3.7 Uhamasishaji wa Vyama vya Ushirika Sinzia

Endapo kutabainika uwepo wa Vyama vya Ushirika Sinzia, wahamasishaji na Maafisa Ushirika watapaswa kufanya tathmini ya kina ili kubaini sababu zilizosababisha vyama hivyo kushindwa kutekeleza shughuli zake ipasavyo. Tathmini hiyo itajumuisha uchambuzi wa hali ya uongozi, ushiriki wa wanachama, mtaji, shughuli za kiuchumi, uzingatiaji wa sheria na migogoro inayoweza kuwa imeathiri utendaji wa chama.

Mpango wa kufufua Vyama Sinzia utajumuisha: -

a) Utambuzi wa Vyama vya Ushirika sinzia
b) Kutoa elimu ya ushirika kwa wanachama na viongozi;
c) Kufanya mikutano ya uhamasishaji na maridhiano kwa wanachama;
d) Kuboresha mifumo ya uongozi na uwajibikaji;
e) Kuandaa au kurekebisha mpango biashara wa chama;
f) Kuhuisha taarifa za chama katika Mfumo wa MUVU;
g) Kuunganisha vyama vinavyofanana pale inapohitajika kwa mujibu wa sheria;
h) Kuwezesha upatikanaji wa masoko, mitaji na huduma za kifedha; na
i) Kufanya ufuatiliaji wa karibu wa utekelezaji wa mpango wa ufufuaji.

Lengo la hatua hizi ni kuhakikisha Vyama Sinzia vinarejea katika utekelezaji wa shughuli zake kwa ufanisi na kuendelea kutoa huduma kwa wanachama wake.

3.8 Uendelezaji wa Vyama vya Ushirika.

Mendeleo ya Chama cha Ushirika yanategemea sana umadhubuti wa ushirikiano baina ya Wanachama, Bodi ya Uongozi na watendaji wa Chama katika utekelezaji wa wajibu wao. Ushirikiano huo unafungamanishwa na nguzo tatu ambazo ni: -

i. Umiliki wa Wanachama (Member Ownership)
ii. Udhibiti wa Wanachama (Member Control) na
iii. Ushiriki wa Wanachama (Member Participation)

Menejimenti (Watendaji) na Bodi ya Uongozi wanapaswa kila wakati kujenga mazingra ya kuwawezesha Wanachama kupiga hatua kuelekea kwenye nguzo hizo.

3.8.1 Umiliki wa Wanachama

Umuhimu wa Mwanachama ndani ya Chama chake unajidhihirisha pale ambapo Mwanachama ametimiza wajibu wake kama ilivyofafanuliwa kwa mujibu wa Sheria na Masharti ya Chama.

Viashiria muhimu vya umiliki wa uanachama ni pamoja na uwiano wa hisa zake katika Chama dhidi ya mtaji wa nje ya Chama.

3.8.2 Udhibiti wa Wanachama

Udhibiti wa Wanachama huweza kudhihirika kupitia nyenzo mbalimbali ukiwemo mchakato wa kuandaa na kupitisha Masharti, Mipango na bajeti, Sera, Miongozo, maazimio ya Wanachama, Taarifa za maendeleo ya Chama zikiwemo taarifa za ukaguzi.

3.8.3 Ushiriki wa Wanachama

Nyenzo kuu za ushiriki wa wanachama ni kushirki na kushirikishwa katika shughuli za Chama, Mikutano, Fursa za kuhudumiwa na Chama na kupata Gawio (Dividends) kutokana na matokeo ya kazi yao ya pamoja.

SEHEMU YA TANO

5.0 HITIMISHO

Ni matarajio ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika kuwa mwongozo huu utarahisisha uratibu wa majukumu ya uhamasishaji, uanzishaji, ufufuaji, uendelezaji na usimamizi wa Vyama vya Ushirika yanayotekelezwa na wadau mbalimbali nchini. Hivyo, watumiaji wa mwongozo huu wanapaswa kuufanyia rejea wakati wote ili kuhakikisha kuwa Vyama vya Ushirika vinaanzishwa, vinaendeshwa na vinaendelezwa kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa, kwa manufaa ya wanachama wake na Taifa kwa ujumla.

VIAMBATISHO

Kiambatisho Na. 1

1. DHANA YA USHIRIKA

Mwananchi anapaswa kufahamu kwamba Ushirika una tafsiri mbili yaani Ushirika kama dhana na Ushirika kama taasisi.

1.1 Ushirika kama Dhana

Mhamasishaji anapaswa kuelewa dhana sahihi ya ushirika kabla ya kuingia katika jukumu la utoaji wa elimu na mafunzo ya ushirika (uhamasishaji). Dhana ya ushirika inajumuisha maeneo makuu matatu ambayo ni pamoja na Maana ya Ushirika; Maadili ya Ushirika na Misingi ya Ushirika.

1.2 Maana ya Ushirika

Ni muungano wa watu walioungana pamoja kwa hiari yao, kwa madhumuni ya kufanikisha mahitaji yao kwa kuazisha, kumiliki na kusimamia chombo chao kidemokrasia na kuchangia mtaji unaohitajika kwa usawa na kukubali kuyakabili matatizo na kupata manufaa kutokana na shughuli zake ambazo wao hushiriki kikamilifu. Watu wanaoanzisha Ushirika hawana budi kuwa na mfungamano wa pamoja, mathalani wakulima wa zao, wakazi wa Kijiji/mtaa, mafundi, Waajiriwa n.k. Kwa mantiki hiyo Vyama vya Ushirika vya aina mbalimbali vinaweza kuanzishwa kulinanga na mahitaji ya walengwa.

1.3 Maadili ya Ushirika

Maadili ya Ushirika Ushirika yamejikita katika kujitegemea, Uwajibikaji, Demokrasia, Haki, Usawa na Mshikamano.

1.4 Misingi ya Ushirika

Uimara na ustawi wa ushirika unategemea sana uzingatiaji wa misingi ya kimataifa ya ushirika. Misingi ya Ushirika ni nguzo muhimu na ni lazima izingatiwe na mhamasishaji katika utoaji wa elimu na mafunzo ili kufikia malengo tarajiwa. Misingi hiyo ni Uanachama

wa hiari na ulio wazi, udhibiti wa kidemokrasia, ushiriki wa wanachama katika shughuli za kiuchumi, uhuru na kujitegemea, elimu, mafunzo na taarifa, ushirikiano miongoni mwa Vyama vya Ushirika na kuijali jamii.

1.5 Ushirika kama Taasisi

Chama cha Ushirika ni taasisi/chombo kinachoundwa na wanachama kwa hiari yao na kusajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika ili kukidhi mahitaji ya Wanachama na jamii. Nchini Tanzania Vyama vya Ushirika vinaundwa kwa kuzingatia Sera ya Maendeleo ya Ushirika iliyopo ambayo inahimiza kuundwa kwa Vyama vya Ushirika kwa kufuata DIRA inayoelekeza uwepo wa Vyama vya Ushirika imara na endelevu vyenye uwezo wa kukidhi mahitaji ya Wanachama ya kiuchumi na kijamii. Sheria ya Vyama vya Ushirika imewekwa ili kutekeleza Sera hiyo.

Kiambatisho Na. 2

2.0 AINA YA VYAMA VYA USHIRIKA VINAVYOWEZA KUANZISHWA

Vyama vya Ushirika vinaweza kuanzishwa kulingana na shughuli mbalimbali za kiuchumi zinazofanyika na ambazo zinahitaji nguvu ya pamoja ili kuleta tija kwa wanachama wake na kuwafanya wamiliki bidhaa/mazao yao hadi wakati wa uuzaji ili kunufaika na matokeo ya kazi yao kupitia ushirika. Sera ya Maendeleo ya Ushirika na Sheria ya Vyama vya Ushirika zimeweka misingi, taratibu na miongozo ya uanzishaji wa aina mbalimbali za Vyama vya Ushirika.

2.1 Ushirika wa Kilimo na Masoko (Agricultural Marketing Cooperative Society): Hushughulika na aina mbalimbali za mazao ya kilimo katika uzalishaji, ununuzi, usindikaji uuzaji, usambazaji wa pembejeo na zana za kilimo pamoja na mambo mengineyo yanayohusu shughuli za kilimo kadri itakavyokuwa imeainishwa katika Masharti ya Chama husika. Ushirika huu utaanzishwa na watu wasipungua ishirini (20) na kuendelea.

2.2 Ushirika wa Akiba na Mikopo (Savings and Credit Cooperative Society-SACCOS): Huu ni ushirika unaowezesha wanachama kujenga tabia ya kuweka akiba na kukopeshana kwa masharti nafuu kwa ajili ya shughuli za kiuchumi na kijamii ambazo ni pamoja na ufugaji, kilimo, ujenzi wa majengo ya biashara, elimu, afya n.k. Ushirika huu utaanzishwa na watu wasiopungua ishirikni (20) na kuendelea.

2.3 Ushirika wa Waalaji (Consumer Cooperative Society): Hujihusisha na utoaji wa huduma zinazohitajika na wanachama, mathalani maduka ya vyakula, nguo, vifaa vya ujenzi, mashine za kusaga, kukoboa na kukamua nafaka n.k. kwa manufaa ya Wanachama wake na jamii kwa ujumla. Ushirika huu utaanzishwa na watu wasiopungua kumi (10) na kuendelea.

2.4 Ushirika wa Viwanda (Industrial Cooperative Society): Ushirika huu hulenga kwenye uanzishaji na uendeshaji wa viwanda vya aina mbalimbali kwa ajili ya kuongeza thamani. Mwanachama ni lazima awe na ujuzi/ufundi unaohitajika. Wanachama wa chama cha ushirika wa viwanda watakuwa ndio wafanyakazi wa kiwanda. Ushirika huu utaanzishwa na watu wasiopungua (10) na kuendelea.

2.5 Ushirika wa Nyumba (Housing Cooperative Society): Ushirika huu huanzishwa kwa nia ya kuwawezesha Wanachama kupata makazi bora pamoja na majengo ya kibiashara. Pia ushirika wa aina hii unaweza kujielekezá katika kutoa huduma ya ujenzi, kumiliki mitambo pamoja na huduma za ushauri wa kitaalamu, ufundi, kutoa vifaa vya ujenzi au kujenga majengo ya kibiashara. Ushirika huu utaanzishwa na watu wasiopungua 10 na kuendelea.

2.6 Ushirika wa Mifugo (livestock Cooperative Society): Ushirika huu huanzishwa ili kuwawezesha Wanachama kukidhi mahitaji yao pamoja na kupata soko bora la mazao ya mifugo. Ushirika yao yanayohusiana na shughuli za ufugaji huu unaweza kujihusisha pia na umiliki wa pamoja wa mifugo, majosho, uuzaji wa Ngozi, unenepeshaji na uchinjaji, usindikaji na uuzaji wa maziwa n.k. unaweza kuanzishwa na watu wasiopungua kumi (10) na kuendelea.

2.7 Ushirika wa Uvuvi (Fisheries Cooperative Society): Ushirika huu unalenga kujihusisha na shughuli za uvuvi, ufugaji wa samaki, upatikanaji wa zana bora za uvuvi, usindikaji wa samaki, utafutaji wa masoko n.k. Unaweza kuanzishwa na watu wasiopungua kumi (10) na kuendelea.

2.8 Ushirika wa Madini (Mining Cooperative Society): Madini ni zao lolote linalopatikana kwa kuchimbuliwa kutoka ardhini, mfano; madini ya vito, chuma, mchanga, mawe, kokoto, n.k. wachimbaji wadogo wadogo na wa kati ili kuweza kufanya Ushirika huu unalenga kuunganisha kazi zao kwa pamoja na kwa tija. Mathalani wachimbaji hawa wanaweza kupata umiliki wa maeneo makubwa kumudu kupata mikopo na mitambo ya kuchimba madini na soko la uhakika la madini. Ushirika huu utaanzishwa na watu wasiopungua kumi (10).

2.9 Ushirika wa Benki (Cooperative Bank): Benki za ushirika ni taasisi zinazoundwa na Wanaushirika ili kuwawezesha kupata mikopo yenye masharti na riba nafuu. Uendeshaji wa vyombo hivi vya kifedha huongozwa na kusimamiwa na sheria mbili ambazo ni Sheria ya Vyama vya Ushirika pamoja na Sheria ya benki na taasisi za fedha. Wanaushirika huanzisha benki za Ushirika kupitia Vyama vyao vya Ushirika kwa

kuwekeza mitaji yao. Kigezo muhimu cha kuweza kusajili benki ni kukidhi matakwa ya Sheria ya benki pamoja na kukidhi mahitaji ya Wanachama yanayokusudiwa.

Tanbihi: Kuna aina nyingi za Vyama vya Ushirika vinavyoweza kuanzishwa kulingana na mahitaji ya wananchi na mazingira husika. Wananchi wanapaswa waelimishwe na kusaidiwa kuibua aina mbalimbali za Vyama vya Ushirika ikiwa ni pamoja na kutumia fursa zinazowazunguka.

Kiambatisho Na. 3

3. Wajibu na Haki ya Mwanachama

3.1 Wajibu

i. Kushiriki katika shughuli zote za kiuchumi zinazohusu chama chake.
ii. Kufuata Sera, Sheria, Kanuni na Masharti ya Chama.
iii. Kulipa kiingilio, kununua hisa, kuweka akiba na amana pamoja na kulipa michango mingine itakayokubaliwa na Wanachama.
iv. Kulinda na kutetea mali za Chama pamoja na kulipa madeni.
v. Kushiriki katika Mikutano ya Chama na kufuata maamuzi yaliyotolewa.
vi. Kudhamini nakulipa mkopo alioudhamini endapo mdhaminiwa ameshindwa kurejesha mkopo huo

3.2 Haki

i. Kusikilizwa
ii. Kuchagua na kuchaguliwa katika nafasi mbalimball za uongozi.
iii. Kupiga kura na kupigiwa kura.
iv. Kuhoji na kupata taarifa zote zinazhusu Chama chake hususani taarifa za ukaguzi na taarifa nyingine muhimu.
v. Kupatiwa taarifa na kuarifiwa kuhusu masuala yote ya Chama.
vi. Kuhudhuria na kushiriki katika Mikutano Mikuu ya Chama.
vii. Kujitoa uanachama.
viii. Kukata rufaa.
ix. Kupata kipato na manufaa mengine yanayotokana na shughuli za biashara ya Chama.
x. Kuteua mrithi kufuatana na Masharti ya Chama.
xi. Kuitisha Mkutano kwa mujibu wa Kanuni na Masharti ya Chama.
xii. Kushiriki katika kuandaa na kurekebisha Masharti ya Chama.
xiii. Kupatiwa hati baada ya kukamilisha malipo yote ya hisa kwa mujibu wa Masharti ya Chama.

Kiambatisho Na. 4

FOMU YA TATHMINI YA UWEZO WA KIUCHUMI ("VIABILITY ASSESSMENT FOR COOPERATIVE SOCIETY") WA CHAMA CHA USHIRIKA.

(Sheria ya Vyama Vya Ushirika (Sura ya 211), Kifungu cha (30)(1)(b)

SEHEMU YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI:

1.1 Jina la Chama: .....

1.2 Anuani ya Chama: ……..…….

1.3 Wilaya ya: .....…….…..…..

1.4 Mkoa wa …….....

1.5 Eneo la Chama .....….....

1.6 Shughuli za chama /Fungamanisho la pamoja (common bond): .....

1.7 Chama kilichopo jirani ……. Umbali (Km): .....

1.8 Asasi/Vikundi vya kijamii vilivyopo: .....

SEHEMU YA PILI

2.0 UANACHAMA*:*

Taarifa za Wanachama

a) Idadi ya watu…..……

b) Idadi ya kaya katika eneo la shughuli ..……

c) Idadi ya watu wazima ……...……

d) Idadi ya vijana ……..…… Me: .....…. Ke: ……..…

e) Uhamiaji wa watu katika eneo la shughuli …….....

f) Idadi ya wanachama waanzilishi ……..…….....

g) Idadi ya wanachama tarajiwa (walionesha nia) ……..……..

h) Sifa za Wanachama ……....……..……

2.2 Taarifa juu ya hali ya kiuchumi

a) Je wanachama wana aina gani ya shughuli za kiuchumi? Ajira/uzalishaji ……

b) Je wanachama wana aina gani ya mapato? .....

c) Masoko

- Ufanisi na ubora wa kibiashara ……..……
- Uwezo wa jamii kufanya manunuzi ……..….
- Uwepo wa masoko ……..…….

Vyanzo vya mapato ya chama itatokana na ……...

3.0 MENEJIMENTI NA UWAJIBIKAJI

a) Upatikanaji wa watendaji

Meneja/katibu …….

Mhasibu/mwekahazina ……..……

Karani ……..……..

Afisa ugani …….

b) Hali ya kijamii

- Uelewa wa Ushirika: ……..…….
- Matarajio ya wanachama: ……..……...

4.0 MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI

MAPATO

- Ushuru ……
- Viingilio ……..…….
- Ruzuku ……..…….……
- Mapato mengineyo ……..……

Jumla ya mapato ……

MATUMIZI

- Samani ……
- Shajala ……
- Posho- Katibu/Meneja ……
- Pango ……
- Gharama za benki ……
- Ada ya mfuko wa ukaguzi ……..……
- Ada ya ukaguzi ……
- Mawasiliano, posta, usafiri ……
- Vikao vya bodi ……
- Mkutano mkuu wa wanachama ……
- Takrima (ukaribisho) ……
- Gharama nyingine ……

Jumla ya matumizi ……

Faida inayotarajiwa ……

5.0 UWEPO WA MAHITAJI YA AWALI KUISAIDIA UFANISI

(a) Huduma mbalimbali

- Huduma za kibenki ……
- Huduma za polisi ……
- Huduma za bima ……
- Huduma za posta ……
- Jengo la ofisi ……
- Samani ……
- Vitendea kazi ……

6.0 MATARAJIO YA KIJAMII NA KIUCHUMI

- Ni matarajio yapi ya kijamii/kiuchumi yanayoweza kupatikana kwa wanachama ……,,,

SEHEMU YA TATU

7.0 MAONI YA AFISA USHIRIKA WA WILAYA

Baada ya kupitia taarifa ya kidadisi uchumi cha chama cha ushirika cha …….. na kuangalia hali ya matarajio ya ufanisi wa uendeshaji wa chama, uwajibikaji na uwezo wa chama kuwa endelevu.

Nina mapendekezo yafuatayo:

- Mapato ya chama yamezidi matumizi kwa ……..%
- Uwiano wa mtaji wa chama unaweza ukakubalika /kutokubalika kukopa kutoka nje na taasisi zinazotoa mikopo.
- Mengine ……

Kutokana na maelezo hapo ju, ninashauri/kutoshauri chama kisajiliwe

....…….. ……..

Muhuri Saini

……..

Tarehe

8.0 MAONI YA MRAJIS MSAIDIZI WA VYAMA VYA USHIRIKA MKOA

Baada ya kupitia taarifa ya kidadisi uchumi cha chama tajwa hapo juu pamoja na mapendekezo kutoka kwa afisa ushirika wa wilaya, nina maoni yafuatayo: ……...

……..…….. ……..……..

Muhuri Saini

……

Tarehe

SEHEMU YA NNE

UAMUZI WA MRAJIS WA VYAMA VYA USHIRIKA

Baada ya kupitia taarifa ya kidadisi uchumi cha chama tajwa hapo juu pamoja na mapendekezo ambayo yanaashiria kusimama kwa kiuchumi kwa chama husika.

Nimeridhika/sijaridhika kuwa chama cha ushirika cha …….. kisajiliwe katika daftari la serikali.

…….. ……..

Muhuri Saini

…….

Tarehe